# Esta

*Malkia Vashti aondolewa*

1 Hili ndilo lililotokea wakati wa utawala wa Mfalme Ahasuero, yule aliyetawala majimbo mia moja na ishirini na saba (127) kutoka Bara Hindi hadi Kushi.

2 Wakati huo Mfalme Ahasuero alitawala kwenye kiti chake cha ufalme katika ngome ya mji wa Shushani.

3 Katika mwaka wa tatu wa utawala wake, alifanya karamu kwa ajili ya wakuu wake wote pamoja na maafisa. Akawaalika viongozi wa jeshi wa Uajemi na Umedi, wana wa wafalme na wakuu wa majimbo.

4 Kwa muda wa siku mia moja na themanini mfalme alionesha utajiri mwingi wa ufalme wake, fahari na utukufu wa enzi yake.

5 Siku hizo zilipopita, mfalme alifanya karamu kwa muda wa siku saba, katika bustani ya ndani katika jumba la kifalme, kwa ajili ya watu wote kuanzia mdogo hadi mkubwa, waliokuwa katika ngome ya mji wa Shushani.

6 Bustani ilikuwa na mapazia ya kitani nyeupe na buluu, yaliyofungiwa kamba za kitani nyeupe na kitambaa cha zambarau, kwenye pete za fedha juu ya nguzo za marumaru. Kulikuwa na viti vya dhahabu na vya fedha vilivyokuwa vimewekwa kwenye ile sakafu iliyotengenezwa kwa mawe ya rangi, marumaru, lulumizi na mawe mengine ya thamani.

7 Vyombo vya dhahabu vilitumika kwa watu kunywea mvinyo, kila kimoja tofauti na kingine, naye mfalme akatoa mvinyo kwa wingi kwa kadiri ya ukarimu wake.

8 Kwa amri ya mfalme kila mgeni aliruhusiwa kunywa alichotaka, kwa kuwa mfalme alitoa maagizo kwa watumishi wote kugawa mvinyo kila mtu kwa jinsi alivyotaka.

9 Malkia Vashti pia akawafanyia wanawake karamu katika jumba la kifalme la Mfalme Ahasuero.

10 Siku ya saba, wakati Mfalme Ahasuero alikuwa amesisimka roho yake kwa mvinyo, aliamuru matowashi saba waliokuwa wakimhudumia, yaani Mehumani, Biztha, Harbona, Bigtha, Abagtha, Zethari na Karkasi,

11 kumleta Malkia Vashti mbele ya mfalme akiwa amevaa taji lake la kifalme, ili aoneshe uzuri wake kwa watu na wakuu, kwa kuwa alikuwa ni mzuri kumtazama.

12 Lakini wakati watumishi walipotoa amri ya mfalme, Malkia Vashti alikataa kuja. Ndipo mfalme alighadhibika, na hasira yake ikawaka.

13 Kwa kuwa ilikuwa desturi ya mfalme kupata ushauri kwa wataalamu katika mambo ya sheria na haki, alizungumza na watu wenye busara, ambao walijua nyakati,

14 nao waliokuwa karibu na mfalme ni Karshena, Shethari, Admatha, Tarshishi, Meresi, Marsena na Memukani, wakuu saba wa Uajemi na Umedi waliokuwa na nafasi ya pekee kwa mfalme nao walikuwa na vyeo vya juu kabisa katika utawala wake.

15 Mfalme akauliza, “Kulingana na sheria, Malkia Vashti anapaswa kutendewa nini? Malkia hakutii amri ya Mfalme Ahasuero ambayo matowashi walimpelekea.”

16 Kisha Memukani akajibu mbele ya mfalme na wakuu, “Malkia Vashti si kwamba amemkosea mfalme tu bali pia amewakosea wakuu wote na watu wa himaya yote ya Mfalme Ahasuero.
17 Kwa maana tendo hili la malkia litajulikana kwa wanawake wote, kwa hiyo watawadharau waume zao na kusema, ‘Mfalme Ahasuero aliagiza Malkia Vashti aletwe mbele yake, lakini alikataa.’
18 Siku ya leo, wanawake wa wakuu wa Uajemi na Umedi ambao wamesikia kuhusu tabia ya malkia watawatendea wakuu wote wa mfalme vivyo hivyo. Hapatakuwa na mwisho wa dharau na ugomvi.

19 “Kwa hiyo, kama itampendeza mfalme, atoe amri ya kifalme na iandikwe katika sheria ya Uajemi na Umedi, ambayo haitabadilika, kwamba Vashti kamwe asije tena mbele ya Mfalme Ahasuero. Pia mfalme na atoe hiyo nafasi yake ya umalkia kwa mwanamke mwingine aliye bora kuliko yeye.
20 Kisha mbiu hii ya mfalme itakapotangazwa katika himaya yake iliyo kubwa sana, wanawake wote watawaheshimu waume zao, kuanzia mdogo hadi mkubwa.”

21 Mfalme na wakuu wake walipendezwa na shauri hili, hivyo basi mfalme akafanya kama Memukani alivyopendekeza.

22 Alipeleka barua katika sehemu zote za
ufalme wake, kwa kila jimbo kwa maandishi
yake mwenyewe na kwa kila watu katika lugha
yao wenyewe, akitangaza kwa msemo wa kila
watu kwamba inampasa kila mwanaume kuwa
mtawala wa nyumba yake mwenyewe.

# 2

*Esta afanywa malkia*

1 Baadaye, wakati hasira ya Mfalme Ahasuero
ilikuwa imetulia, alimkumbuka Vashti na kile ali-
chokuwa amekifanya, na alilokuwa ameamuru
juu yake.
2 Kisha watumishi waliomhudumia mfalme
walipendekeza, “Watafutwe wanawali mabikira
wazuri wa sura kwa ajili ya mfalme.
3 Mfalme na awateue maafisa katika kila
jimbo la himaya yake kuwaleta hao wanawali
wote wazuri wa sura katika nyumba ya
wanawake katika ngome ya mji wa Shushani.
Kisha wawekwe chini ya uangalizi wa Hegai,
towashi wa mfalme, aliyekuwa msimamizi wa
wanawake; na wapewe huduma zote za urembo.
4 Kisha yule ambaye atampendeza mfalme na
awe malkia badala ya Vashti.” Shauri hili likam-
pendeza mfalme, naye akalifuata.

5 Basi katika mji wa ngome ya Shushani pa-
likuwa na Myahudi wa kabila la Benyamini,
jina lake Mordekai mwana wa Yairi, mwana wa
Shimei, mwana wa Kishi,
6 ambao walichukuliwa uhamishoni kutoka
Yerusalemu na Mfalme Nebukadneza wa Babeli,

wakiwa miongoni mwa waliochukuliwa mateka
pamoja na Mfalme Yekonia wa Yuda.
7 Mordekai alikuwa na binamu yake msichana
aliyeitwa Hadasa, ambaye alimlea kwa kuwa
hakuwa na baba wala mama. Msichana huyu,
ambaye pia alijulikana kwa jina la Esta, alikuwa
na umbo na sura ya kupendeza, naye Mordekai
alimtunza kama binti yake mwenyewe baada ya
baba yake na mama yake kufariki.
8 Agizo na amri ya mfalme ilipotangazwa,
wanawali wengi waliletwa kwenye ngome ya
mji wa Shushani na kuwekwa chini ya uangalizi
wa Hegai. Pia Esta alipelekwa katika jumba la
mfalme na akakabidhiwa kwa Hegai, aliyekuwa
mkuu wa nyumba ya wanawake.
9 Msichana huyu alimpendeza na kupata kibali
mbele zake. Mara moja akaanza kumpa matunzo
ya urembo na chakula maalum. Alimpa Esta
vijakazi saba waliochaguliwa kutoka jumba la ki-
falme, na kumhamishia yeye pamoja na vijakazi
wake katika sehemu bora zaidi katika nyumba ya
wanawake.
10 Esta alikuwa hajadhihirisha uraia wake
na asili yake, kwa sababu Mordekai alikuwa
amemkataza kufanya hivyo.
11 Kila siku Mordekai alikuwa akitembeatem-
bea karibu na ua wa nyumba ya wanawake
kujua Esta alivyoendelea na kuona yaliyokuwa
yakitendeka kwake.
12 Kabla zamu ya msichana haijafika ya
kwenda kwa Mfalme Ahasuero, ilimbidi atimize
miezi kumi na mbili ya matunzo ya urembo
kama ilivyokuwa imepangwa. Kwa miezi sita

walikuwa wajipake mafuta ya manemane, na
miezi sita kujipaka manukato na vipodozi.
13 Basi hivi ndivyo ambavyo msichana
angeingia kwa mfalme: Kila kitu alichohitaji
aliruhusiwa kuchukua kutoka nyumba ya
wanawake na kwenda navyo katika jumba la
mfalme.
14 Jioni angeenda pale na asubuhi kurudi se-
hemu nyingine ya nyumba ya wanawake katika
utunzaji wa Shaashgazi, towashi wa mfalme
aliyekuwa mkuu wa masuria. Hangeweza ku-
rudi kwa mfalme hadi apendezwe naye na kuag-
iza aitwe kwa jina lake.

15 Zamu ya Esta ilipofika kwenda kwa mfalme
(msichana ambaye Mordekai alikuwa amemlea,
binti Abihaili, mjomba wake), Esta hakutaka
vitu zaidi ya vile Hegai, towashi wa mfalme
aliyekuwa mkuu wa nyumba ya wanawake,
alikuwa amemshauri. Naye Esta alipata kibali
kwa kila mtu aliyemwona.
16 Esta alipelekwa kwa Mfalme Ahasuero
katika makao ya mfalme mwezi wa kumi, yaani
mwezi wa Tebethi, katika mwaka wake wa saba
wa kutawala.
17 Basi mfalme alivutiwa na Esta kuliko
wanawake wengine wote, naye akapata upen-
deleo na kibali kuliko mabikira wengine. Kisha
akamvika taji la kifalme kichwani mwake na
kumfanya malkia badala ya Vashti.
18 Mfalme akafanya karamu kubwa, karamu ya
Esta, kwa wakuu wake wote na maafisa. Mfalme
akatangaza siku ya mapumziko katika majimbo
yake yote na kugawa zawadi kwa ukarimu wa

kifalme.

*Mordekai agundua hila*

19 Wakati mabikira walikusanyika mara ya
pili, Mordekai alikuwa ameketi katika lango la
mfalme.
20 Lakini Esta alikuwaameficha siri ya asili
yake na uraia wake, kama Mordekai alivyokuwa
amemwambia, kwa maana aliendelea kufuata
maelekezo ya Mordekai kama alivyokuwa aki-
fanya alipokuwa akimlea.
21 Ikawa Mordekai alipokuwa ameketi kwenye
lango la mfalme, Bigthana na Tereshi, maafisa
wawili wa mfalme waliokuwa walinzi wa lango,
walikasirika na kupanga njama ya kumuua
Mfalme Ahasuero.
22 Lakini Mordekai aligundua hila hii na
kumwambia Malkia Esta, ambaye baadaye al-
imwarifu mfalme, huku akimsifu Mordekai.
23 Taarifa hiyo ilipochunguzwa na kuonekana
kuwa kweli, maafisa hao wawili waliangikwa juu
ya miti ya kunyongea. Haya yote yaliandikwa
katika kitabu cha kumbukumbu mbele ya
mfalme.

# 3

*Hila ya Hamani kuwaangamiza Wayahudi*

1 Baada ya matukio haya, Mfalme Ahasuero
alimheshimu Hamani mwana wa Hamedatha
Mwagagi, akampandisha na kumpa kiti chake
cha heshima cha juu sana kuliko wakuu wengine
wote.
2 Maafisa wote wa mfalme waliokaa langoni
mwa mfalme walipiga magoti na kumpa Hamani

heshima, kwa kuwa mfalme alikuwa ameamuru hili kuhusu Hamani. Lakini Mordekai hakumpigia magoti wala kumheshimu.

3 Kisha maafisa wa mfalme waliokuwa langoni mwa mfalme walimuuliza Mordekai, “Kwa nini hutii agizo la mfalme?”

4 Siku baada ya siku walizungumza naye lakini hakukubali. Kwa hiyo walimweleza Hamani kuona kama tabia ya Mordekai itaweza kuvumiliwa, kwa maana alikuwa amewaambia kuwa yeye ni Myahudi.

5 Hamani alipoona kuwa Mordekai hampigii magoti wala kumpa heshima, alighadhibika.

6 Hata hivyo, baada ya kujulishwa watu wa Mordekai ni akina nani, alibadili wazo la kumuua Mordekai peke yake. Badala yake Hamani alitafuta njia ya kuwaangamiza watu wote wa Mordekai, yaani Wayahudi, walio katika ufalme wote wa Ahasuero.

7 Katika mwaka wa kumi na mbili wa utawala wa Mfalme Ahasuero, katika mwezi wa kwanza uitwao Nisani, walipiga puri (yaani kura) mbele ya Hamani ili kuchagua siku na mwezi. Kura ikaangukia kwenye mwezi wa kumi na mbili, yaani Adari.

8 Kisha Hamani akamwambia Mfalme Ahasuero, “Wako watu fulani wameenea na kutawanyika miongoni mwa watu katika majimbo yote ya ufalme wako, ambao desturi zao ni tofauti na zile za watu wengine wote, nao hawatii sheria za mfalme. Haifai mfalme kuwavumilia watu hawa.

9 Kama inampendeza mfalme, itolewe amri kuwaangamiza, nami nitaweka talanta elfu

kumi* za fedha katika hazina ya mfalme kwa ajili ya watu watakaoshughulikia jambo hili.”

10 Basi mfalme alichukua pete yake ya muhuri kutoka kidole chake na kumpa Hamani mwana wa Hamedatha Mwagagi, adui wa Wayahudi.

11 Mfalme akamwambia Hamani, “Baki na fedha yako na uwatendee hao watu utakavyo.”

12 Kisha siku ya kumi na tatu ya mwezi wa kwanza waandishi wa mfalme waliitwa. Wakaandika barua kwa kila jimbo na katika kila lugha ya watu kama agizo la Hamani lilivyotoka kwa mfalme, kwa watawala wa majimbo mbalimbali, na wakuu wa watu mbalimbali. Hizi ziliandikwa kwa jina la Mfalme Ahasuero mwenyewe na kutiwa muhuri wa pete yake mwenyewe.

13 Barua zilipelekwa na tarishi katika majimbo yote ya mfalme zikiwa na amri ya kuharibu, kuua na kuangamiza Wayahudi wote, wadogo kwa wakubwa, wanawake na watoto wadogo, siku moja, yaani siku ya kumi na tatu ya mwezi wa kumi na mbili, ndio mwezi wa Adari, na pia kuteka nyara vitu vyao.

14 Nakala ya andiko la amri ilipaswa kutolewa kama sheria katika kila jimbo, na kufahamishwa kwa watu wa kila taifa ili waweze kuwa tayari kwa siku ile.

15 Kwa kuharakishwa na amri ya mfalme, matarishi walienda na andiko lilitolewa katika mji wa ngome ya Shushani. Mfalme na Hamani waliketi na kunywa, lakini mji wa Shushani ulifadhaika.

---

* **3:9** Talanta 10,000 ni sawa na tani 340.

# 4

### *Mordekai amshawishi Esta kusaidia*

1 Mordekai alipojua yote yaliyokwisha ku-
fanyika, alirarua mavazi yake, akavaa magunia
na kujipaka majivu, akaenda mjini akiomboleza
kwa sauti na kwa uchungu.
2 Alienda na kusimama nje ya lango la mfalme,
kwa sababu hakuna yeyote aliyeruhusiwa kuin-
gia akiwa amevaa magunia.
3 Katika kila jimbo ambapo amri na agizo la
mfalme lilifika, kulikuwa na maombolezo makuu
miongoni mwa Wayahudi pamoja na kufunga,
kulia na kuomboleza. Watu wengi wakalala juu
ya magunia na majivu.
4 Wajakazi wa Esta na matowashi walipokuja
na kumwambia kuhusu Mordekai, alipatwa na
huzuni kuu. Alimtumia nguo avae badala ya
magunia, lakini Mordekai hakuzikubali.
5 Ndipo Esta akamwita Hathaki, mmoja wa
matowashi wa mfalme aliyekuwa amewekwa
kumhudumia Esta, akamwagiza kutafuta kili-
chokuwa kikimtaabisha Mordekai na ni kwa
nini.
6 Basi Hathaki alitoka nje kumwendea
Mordekai kwenye uwanja ulio wazi wa mji
mbele ya lango la mfalme.
7 Mordekai akamwambia kila kitu ambacho
kimempata, pamoja na hesabu kamili ya fedha
ambazo Hamani aliahidi kulipa katika hazina ya
mfalme kwa ajili ya maangamizi ya Wayahudi.
8 Akampa nakala ya andiko la amri kwa ajili ya
maangamizi yao, lililokuwa limechapishwa huko
Shushani, kumwonesha Esta na kumwelezea.

Mordekai akamwambia towashi amshawishi Esta kwenda mbele ya mfalme kuomba rehema na kumsihi kwa ajili ya watu wake.

9 Hathaki akarudi kwa Esta na kumwarifu alilolisema Mordekai.

10 Kisha Esta akamwamuru Hathaki amweleze Mordekai,

11 "Maafisa wote wa mfalme na watu wa majimbo ya ufalme wanajua kuwa mwanaume au mwanamke yeyote ambaye ataingia kumwona mfalme katika ua wa ndani bila kuitwa, mfalme ana sheria moja tu: Atauawa. Njia pekee kinyume na hili ni mfalme kumnyooshea fimbo ya dhahabu ili aishi. Lakini siku thelathini zimepita tangu nilipoitwa kwenda kwa mfalme."

12 Wakati Mordekai aliarifiwa maneno ya Esta,

13 Mordekai alirudisha jibu hili: "Usifikiri kwamba kwa sababu uko katika nyumba ya mfalme wewe pekee katika Wayahudi wote utapona.

14 Kwa kuwa kama utakaa kimya wakati huu, msaada na ukombozi kwa Wayahudi utatoka mahali pengine, lakini wewe na jamaa ya baba yako mtaangamia. Nani ajuaye kwamba hukuja kwenye nafasi ya mamlaka kwa ajili ya wakati kama huu?"

15 Kisha Esta alituma jibu hili kwa Mordekai:

16 "Nenda, wakusanye Wayahudi wote walio Shushani, nanyi mfunge kwa ajili yangu. Msile wala kunywa kwa siku tatu, usiku na mchana. Mimi na wajakazi wangu tutafunga kama mnavyofanya. Baada ya kufanyika hili, nitaenda kwa mfalme, hata ingawa ni kinyume cha sheria. Ikiwa ni kuangamia na niangamie."

17 Kwa hiyo Mordekai alienda zake na
kutekeleza maagizo yote ya Esta.

# 5

*Ombi la Esta kwa mfalme*

1 Siku ya tatu, Esta alivaa mavazi yake ya ki-
malkia, naye akasimama katika ua wa ndani wa
jumba la mfalme, mbele ya ukumbi wa mfalme.
Naye mfalme alikuwa ameketi kwenye kiti chake
cha kifalme katika ukumbi, akielekea langoni.
2 Alipomwona Malkia Esta amesimama uani
alipendezwa naye, akamnyooshea fimbo ya
utawala ya dhahabu iliyokuwa mkononi mwake.
Kwa hiyo Esta alikaribia na kuigusa ncha ya
fimbo ya mfalme.
3 Kisha mfalme aliuliza, "Malkia Esta, ni nini?
Ombi lako ni nini? Hata kama ni nusu ya ufalme,
utapewa."
4 Esta akajibu, "Kama itampendeza mfalme,
mfalme pamoja na Hamani waje leo katika
karamu niliyomwandalia."
5 Mfalme akasema, "Mleteni Hamani mara
moja, ili tupate kufanya lile Esta analoomba."

Kwa hiyo mfalme na Hamani walihudhuria karamu aliyoiandaa Esta.

6 Walipokuwa wakinywa mvinyo mfalme aka-
muuliza Esta tena, "Sasa haja yako ni nini?
Utapewa. Ombi lako ni nini? Hata nusu ya
ufalme, utapewa."
7 Esta akajibu, "Haja yangu na ombi langu ni
hili:

8 Kama mfalme ameona vyema, nami nimepata kibali kwake, na ikimpendeza mfalme kunipa ombi langu na kunitimizia haja yangu, mfalme na Hamani waje kwangu kesho katika karamu nitakayowaandalia. Kisha nitajibu swali la mfalme."

### *Ghadhabu ya Hamani dhidi ya Mordekai*

9 Hamani alitoka siku hiyo kwa furaha na moyo mchangamfu. Lakini alipomwona Mordekai langoni mwa mfalme na kuona kwamba hakusimama wala hakuonesha hofu mbele yake, alijawa na ghadhabu dhidi ya Mordekai.
10 Hata hivyo, Hamani alijizuia akaenda zake nyumbani.

Akawaita pamoja rafiki zake na Zereshi, mkewe.
11 Hamani akajisifia kwao juu ya utajiri wake mwingi, wanawe wengi na kwa njia zote ambazo mfalme amemheshimu kwazo na jinsi alivyomweka juu ya wakuu na maafisa wengine.
12 Hamani akaongeza, "Si hayo tu. Mimi ndiye mtu pekee ambaye Malkia Esta amemwalika kumsindikiza mfalme kwenye karamu aliyomwandalia. Naye amenialika pamoja na mfalme kesho.
13 Lakini haya yote hayanipi kuridhika iwapo ninaendelea kumwona yule Myahudi Mordekai akiketi kwenye lango la mfalme."
14 Zereshi mkewe na rafiki zake wote wakamwambia, "Tengeneza mahali pa kuangika watu kimo chake dhiraa hamsini*, kisha kesho

* **5:14** Dhiraa 50 ni sawa na mita 22.5.

asubuhi mwombe mfalme Mordekai aangikwe juu yake. Ndipo uende na mfalme kwenye karamu kwa furaha." Shauri hili lilimpendeza Hamani, naye akajenga mahali pa kuangika watu.

# 6

*Mordekai anapewa heshima*

1 Usiku ule mfalme hakupata usingizi, hivyo
akaagiza aletewe kitabu cha kumbukumbu za
matukio ya utawala wake, asomewe.
2 Ikaonekana imeandikwa humo kwamba
Mordekai alikuwa amefichua jinsi Bigthana na
Tereshi, waliokuwa maafisa wawili wa mfalme,
walinzi wa lango walivyokuwa wamepanga hila
ya kumuua Mfalme Ahasuero.
3 Mfalme akauliza, "Je, ni heshima na shukrani
gani Mordekai alipokea kwa ajili ya jambo hili?"

Watumishi wake wakajibu, "Hakuna lolote alilotendewa."

4 Mfalme akasema, "Ni nani yuko uani?" Wakati
huo huo Hamani alikuwa ameingia kwenye ua
wa nje wa jumba la mfalme kusema na mfalme
kuhusu kumwangika Mordekai katika mahali pa
kuangikia watu alipokuwa amepajenga kwa ajili
yake.
5 Watumishi wake wakamjibu, "Hamani ames-
imama uani."

Mfalme akaamuru, "Mleteni ndani."

6 Hamani alipoingia, mfalme alimuuliza,
"Afanyiwe nini mtu ambaye mfalme apenda
kumheshimu?"

Basi Hamani akawaza moyoni mwake, “Ni nani
mwingine ambaye mfalme angemheshimu ku-
liko mimi?”
7 Kwa hiyo akamjibu mfalme, “Kwa mtu am-
baye mfalme apenda kumheshimu,
8 aletewe joho la kifalme ambalo mfalme
ameshalivaa na farasi ambaye mfalme alisham-
panda, ambaye amevikwa taji la kifalme kich-
wani mwake.
9 Kisha joho na farasi vikabidhiwe kwa
mmoja wa wakuu wa mfalme anayeheshimika
sana. Nao wamvike mtu yule ambaye mfalme
anapenda kumheshimu, na aongozwe akiwa juu
ya farasi kupitia barabara za mji, wakitangaza
mbele yake, ‘Hivi ndivyo anavyotendewa mtu
ambaye mfalme apenda kumheshimu!’ ”

10 Mfalme akamwamuru Hamani, “Nenda mara
moja, chukua joho na farasi na ufanye kama
vile ulivyopendekeza kwa Mordekai Myahudi,
akaaye langoni mwa mfalme. Usipuuze kufanya
kitu chochote ulichoshauri.”

11 Hivyo Hamani akachukua joho na farasi.
Akamvika Mordekai, na kumpandisha juu
ya farasi, akamtembeza katika barabara za
mji akitangaza mbele yake, “Hivi ndivyo
anavyotendewa mtu ambaye mfalme anapenda
kumheshimu!”

12 Baadaye Mordekai akarudi kwenye lango la
mfalme. Lakini Hamani akakimbia nyumbani,
akiwa amejaa huzuni,
13 naye akamweleza Zereshi mkewe pamoja na
rafiki zake wote kila kitu ambacho kimempata.

Washauri wake pamoja na Zereshi mkewe wakamwambia, “Kwa kuwa Mordekai, ambaye mbele yake umeanza kuanguka ni wa asili ya Kiyahudi, huwezi kushindana naye; kwa hakika utaanguka!”
14 Walipokuwa bado wakizungumza naye, matowashi wa mfalme wakaja na kumharakisha Hamani aende katika karamu aliyoiandaa Esta.

# 7

*Hamani aangikwa*

1 Basi mfalme na Hamani wakaenda kula chakula pamoja na Malkia Esta.
2 Walipokuwa wakinywa mvinyo katika siku ya pili, mfalme akauliza tena, “Malkia Esta, ni nini haja yako? Utapewa. Ombi lako ni nini? Hata nusu ya ufalme, utapewa.”
3 Kisha Malkia Esta akajibu, “Kama nimepata kibali kwako, ee mfalme, tena kama inapendeza utukufu wako, nijalie maisha yangu, hii ndiyo haja yangu. Pia uokoe watu wangu, hili ndilo ombi langu.
4 Kwa kuwa mimi na watu wangu tumeuzwa ili tuangamizwe, tuchinjwe na tuharibiwe. Tungeuzwa tu kama watumwa wa kiume na wa kike, ningenyamaza, kwa sababu shida kiasi hicho haingetosha kumsumbua mfalme.”
5 Mfalme Ahasuero akamuuliza Malkia Esta, “Ni nani huyu? Yuko wapi mtu huyu aliyethubutu kufanya jambo kama hili?”
6 Esta akasema, “Mtesi na adui ni huyu mwovu Hamani.”

Hamani alifadhaika mbele ya mfalme na malkia.
7 Mfalme akainuka kwa ghadhabu, akaacha mvinyo wake, akaenda kwenye bustani ya jumba la kifalme. Lakini Hamani, akitambua kwamba mfalme ameshaamua hatima yake, alibaki nyuma kumsihi Malkia Esta aokoe maisha yake.

8 Mara mfalme aliporudi kutoka bustani ya jumba la kifalme na kuingia kwenye ukumbi wa karamu, Hamani alikuwa akijitupa kwenye kiti kile Esta alikuwa akiegemea.

Mfalme akasema kwa nguvu, "Je, atamdhalilisha malkia hata huku nyumbani akiwa pamoja nami!"

Mara neno lilipotoka kinywani mwa mfalme, walifunika uso wa Hamani.
9 Kisha Harbona, mmoja wa matowashi waliomtumikia mfalme, akasema, "Mahali pa kuangika watu penye urefu wa dhiraa hamsini* pako nyumbani mwa Hamani. Alikuwa amepatengeneza kwa ajili ya Mordekai, ambaye alizungumza ili kumsaidia mfalme."

Mfalme akasema, "Mwangikeni juu yake!"
10 Kwa hiyo wakamtundika Hamani mahali alipokuwa ameandaa kwa ajili ya Mordekai. Ndipo ghadhabu ya mfalme ikatulia.

# 8

*Amri ya mfalme kuhusu Wayahudi*

* **7:9** Dhiraa hamsini ni kama mita 22.

1 Siku ile ile Mfalme Ahasuero akampa Malkia
Esta shamba la Hamani, adui wa Wayahudi.
Naye Mordekai akaja mbele ya mfalme, kwa
kuwa Esta alikuwa amesema jinsi anavyohu-
siana naye.
2 Mfalme akaivua pete yake ya muhuri,
ambayo alikuwa amemnyang'anya Hamani,
akampa Mordekai, naye Esta akamweka
Mordekai asimamie shamba la Hamani.
3 Esta alimsihi tena mfalme, akianguka migu-
uni pake na kulia. Akamwomba akomeshe
mpango mwovu wa Hamani Mwagagi ambao
alikuwa ameupanga dhidi ya Wayahudi.
4 Kisha mfalme alimnyooshea Esta fimbo yake
ya utawala ya dhahabu naye aliinuka na kusi-
mama mbele yake.
5 Esta akasema, "Ikimpendeza mfalme, nami
nikipata kibali, naye akiona ni jambo lililo
sawa kunitendea, na akipendezwa nami, basi
iandikwe amri ya kuzitangua barua zile Hamani
mwana wa Hamedatha Mwagagi, alizotunga na
kuandika kuangamiza Wayahudi katika majimbo
yote ya mfalme.
6 Kwa maana nitawezaje kuvumilia kuona
maafa yakiwapata watu wangu? Nitawezaje
kuvumilia kuona maangamizi ya jamaa zangu?"
7 Mfalme Ahasuero akawajibu Malkia Esta
na Mordekai Myahudi, "Kwa sababu Hamani
aliwashambulia Wayahudi, nimetoa shamba la
Hamani kwa Esta, naye ameangikwa kwenye mti
wa kunyongea.
8 Basi andika amri nyingine kwa jina la mfalme
kwa ajili ya Wayahudi kama unavyoona vyema,

kisha uifunge kwa kutia muhuri kwa pete ya mfalme kwa kuwa hakuna andiko lililoandikwa kwa jina la mfalme na kutiwa muhuri kwa pete ya mfalme linaloweza kutanguliwa.”

9 Mara moja waandishi wa mfalme wakaitwa
kwenye siku ya ishirini na tatu, mwezi wa
tatu, ndio mwezi wa Siwani. Wakaandika yote
Mordekai aliyoamuru kwa Wayahudi, kwa ma-
jemadari, watawala na wakuu wa majimbo mia
moja na ishirini na saba (127) kuanzia Bara Hindi
hadi Kushi. Maagizo haya yaliandikwa kwa
maandishi ya kila jimbo na kwa lugha ya kila mtu
pia kwa Wayahudi kwa maandishi yao wenyewe
na lugha yao.

10 Mordekai aliandika nyaraka kwa jina la
Mfalme Ahasuero, akazitia muhuri kwa pete
ya mfalme na kuzipeleka kwa matarishi, am-
bao waliendesha farasi wepesi waliozalishwa
maalum kwa ajili ya mfalme.

11 Waraka wa mfalme uliwaruhusu Wayahudi
katika kila mji kuwa na haki ya kukusanyika
na kujilinda wenyewe; kuharibu, kuua na
kuangamiza jeshi lolote, taifa lolote au jimbo lile
litakalowashambulia wao, wake zao, watoto wao
na kuteka mali ya adui zao.

12 Siku ambayo iliwekwa kwa Wayahudi ku-
fanya hili katika majimbo yote ya Mfalme Aha-
suero ilikuwa siku ya kumi na tatu ya mwezi wa
kumi na mbili, yaani mwezi wa Adari.

13 Nakala ya tangazo ilikuwa itolewe kama
sheria katika kila jimbo na iweze kujulikana kwa
watu wa kila taifa, ili Wayahudi wawe tayari siku
hiyo kulipiza kisasi kwa adui zao.

14 Matarishi, wakiwa wamepanda farasi wa
kifalme, walitoka mbio wakichochewa na agizo
la mfalme. Tangazo lilitolewa pia katika ngome
ya mji wa Shushani.

*Ushindi wa Wayahudi*

15 Mordekai akaondoka mbele ya mfalme
akiwa amevaa mavazi ya kifalme ya buluu na
nyeupe, taji kubwa la dhahabu na joho la zam-
barau la kitani safi. Na mji wa Shushani ukash-
erehekea kwa furaha.
16 Kwa maana kwa Wayahudi ulikuwa wakati
wa raha na furaha, shangwe na heshima.
17 Katika kila jimbo na katika kila jiji, popote
waraka wa mfalme ulipofika, kulikuwa na
furaha na shangwe miongoni mwa Wayahudi,
pamoja na karamu na kushangilia. Na watu
wengi wa mataifa mengine wakajifanya
Wayahudi kwa sababu ya kuwahofu Wayahudi.

# 9

1 Katika siku ya kumi na tatu ya mwezi wa kumi
na mbili, yaani mwezi wa Adari, amri iliyoagizwa
na mfalme ilikuwa itekelezwe. Siku hii adui wa
Wayahudi walikuwa wametumaini kuwashinda,
lakini sasa mambo yaliwageukia na Wayahudi
wakawashinda wale waliokuwa wanawachukia.
2 Wayahudi walikusanyika katika miji
yao, katika majimbo ya Mfalme Ahasuero
kuwashambulia wale waliokuwa wanatafuta
kuwaangamiza. Hakuna yeyote aliyeweza
kushindana nao, kwa sababu watu wa mataifa
mengine yote waliwaogopa.

3 Nao wakuu wote wa majimbo, majemadari,
watawala na maafisa wa mfalme wakawasaidia
Wayahudi, kwa sababu walimhofu Mordekai.
4 Mordekai alikuwa mtu mashuhuri katika
jumba la mfalme; sifa zake zilienea katika ma-
jimbo yote naye alipata uwezo zaidi na zaidi.
5 Wayahudi waliwaangusha adui zao wote kwa
upanga wakiwaua na kuwaangamiza, nao wali-
fanya kile walichotaka kwa wale waliowachukia.
6 Katika ngome ya Shushani Wayahudi waliua
na kuangamiza wanaume mia tano.
7 Pia waliwaua Parshendatha, Dalfoni, As-
patha,
8 Poratha, Adalia, Ardatha,
9 Parmashta, Arisai, Aridai na Waizatha,
10 wana kumi wa Hamani mwana wa Hame-
datha, adui wa Wayahudi. Lakini hawakuchukua
nyara.
11 Mfalme aliarifiwa siku hiyo hiyo hesabu ya
waliouawa katika ngome ya Shushani.
12 Mfalme akamwambia Malkia Esta,
“Wayahudi wamewaua wanaume mia tano,
na wana kumi wa Hamani ndani ya ngome
ya Shushani. Wamefanyaje katika majimbo
mengine ya mfalme yaliyobaki? Je, sasa haja
yako ni nini? Nayo pia utapewa. Nalo ombi lako
ni nini? Nalo utatendewa.”
13 Esta akajibu, “Ikimpendeza mfalme, uwape
ruhusa Wayahudi walio Shushani warudie amri
ya leo kesho pia, na wana wa Hamani kumi
wanyongwe mahali pa kunyongea watu.”
14 Basi mfalme akaamuru kwamba hili liten-
deke. Amri ilitolewa huko Shushani, nao
wakawanyonga wana kumi wa Hamani.

15 Wayahudi huko Shushani wakakusanyika
pamoja siku ya kumi na nne ya mwezi wa
Adari, nao wakawaua wanaume mia tatu huko
Shushani, lakini hawakuchukua nyara zao.
16 Wakati ule ule, Wayahudi wengine
waliokuwa kwenye majimbo ya mfalme,
wakakusanyika kujilinda nao wakapata nafuu
kutokana na adui zao. Waliua adui zao wapatao
elfu sabini na tano, lakini hawakugusa nyara
zao.
17 Hili lilitendeka siku ya kumi na tatu ya
mwezi wa Adari na siku ya kumi na nne
walipumzika na kuifanya siku ya karamu na
furaha.

*Kusherehekea Purimu*

18 Wayahudi huko Shushani, hata hivyo, wa-
likuwa wamekusanyika siku ya kumi na tatu
na ya kumi na nne, pia siku ya kumi na tano
walipumzika na kuifanya siku ya karamu na
furaha.
19 Ndiyo sababu Wayahudi wanaokaa vijijini
na katika miji midogo huadhimisha siku ya kumi
na nne ya mwezi wa Adari kama siku ya furaha
na karamu, siku ambayo wao hupeana zawadi
mmoja kwa mwingine.

*Purimu kuadhimishwa*

20 Mordekai aliandika matukio haya, naye
akapeleka barua kwa Wayahudi wote walio
katika majimbo ya Mfalme Ahasuero, majimbo
yaliyo mbali na karibu,
21 akiwataka kila mwaka washerehekee siku ya
kumi na nne na ya kumi na tano ya mwezi wa
Adari

22 kama wakati ambao Wayahudi walipata
nafuu kutoka kwa adui zao na kama mwezi
ambao huzuni yao iligeuzwa kuwa furaha na
kuomboleza kwao kuwa siku ya kusherehekea.
Aliwaandikia kushika siku hizo kama siku za
karamu na za furaha na kupeana zawadi za
vyakula wao kwa wao na zawadi kwa maskini.
23 Hivyo Wayahudi walikubali kuendeleza
sherehe walizokuwa wamezianza, wakifanya lile
Mordekai alilokuwa amewaandikia.
24 Kwa maana Hamani mwana wa Hamedatha
Mwagagi, adui wa Wayahudi wote, alikuwa
amepanga hila dhidi ya Wayahudi ili
kuwaangamiza, na alikuwa amepiga *puri* (yaani
kura) kwa ajili ya maangamizi na uharibifu wao.
25 Lakini wakati shauri hilo baya lilipoarifiwa
kwa mfalme, alitoa amri iliyoandikwa kwamba
mipango mibaya ambayo Hamani ameipanga
dhidi ya Wayahudi inapasa imrudie juu ya
kichwa chake mwenyewe, na kwamba yeye na
wanawe waangikwe mahali pa kunyongea watu.
26 (Kwa hiyo siku hizi ziliitwa Purimu, ku-
tokana na neno *puri*.) Kwa sababu ya kila kitu
kilichoandikwa kwenye barua hii na kwa sababu
ya yale waliyoyaona na yale yaliyowatokea,
27 Wayahudi wakachukua na kuimarisha des-
turi kwamba wao na wazao wao na wote ambao
walijiunga nao wangezishika siku hizi mbili kila
mwaka bila kuacha, kwa njia ilivyoelekezwa na
kwa wakati wake.
28 Siku hizi zinapasa zikumbukwe na kuad-
himishwa katika kila kizazi, kila jamaa na
katika kila jimbo na kila jiji. Nazo siku hizi
za Purimu kamwe zisikome kusherehekewa na

Wayahudi, wala kumbukumbu zake zisipotee
miongoni mwa wazao wake.
29 Basi Malkia Esta binti Abihaili, pamoja
na Mordekai Myahudi, waliandika kwa mam-
laka yote kuthibitisha barua hii ya pili kuhusu
Purimu.
30 Naye Mordekai akatuma barua kwa
Wayahudi wote katika majimbo mia moja na
ishirini na saba (127) ya ufalme wa Ahasuero,
barua zenye maneno ya amani na matumaini,
31 ili kuimarisha siku hizi za Purimu katika ma-
jira yake yaliyowekwa, kama Mordekai Myahudi
na Malkia Esta walivyowaamuru, na walivy-
ojiimarisha wenyewe na wazao wao kuhusu
nyakati za kufunga na kuomboleza.
32 Amri ya Esta ilithibitisha taratibu hizi
kuhusu Purimu, nayo ikaandikwa katika kum-
bukumbu.

# 10

*Ukuu wa Mordekai*

1 Mfalme Ahasuero alitoza ushuru katika hi-
maya yake yote, hadi miambao yake ya mbali.
2 Na kuhusu matendo yake yote ya nguvu
na uwezo, pamoja na habari zote za ukuu wa
Mordekai ambao mfalme alikuwa amempan-
disha, je, hayakuandikwa katika kitabu cha kum-
bukumbu za wafalme wa Umedi na Uajemi?
3 Mordekai Myahudi alikuwa wa pili kwa cheo
baada ya Mfalme Ahasuero, naye alikuwa bora
kabisa na mkuu miongoni mwa Wayahudi. Al-
iheshimiwa sana na Wayahudi wenzake wengi,

kwa sababu alifanya kazi kwa manufaa ya watu wake na kutetea ustawi wa Wayahudi wote.

# Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu

## The Holy Bible in Swahili: Open Neno: Maandiko Matakatifu 2024

copyright © 2018, 2024 Biblica, Inc.

Language: Kiswahili (Swahili)

Contributor: Biblica, Inc.

Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu™ ONMM™
Hakimiliki © 2018, 2024 na Biblica, Inc.
Biblica® Open Kiswahili Contemporary Scriptures™
Copyright © 2018, 2024 by Biblica, Inc.

**Creative Commons License**

Kazi hii imewezeshwa kupitia idhini ya kundi la the Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0 International License (CC BY-SA). Ili kuona nakala ya idhini hii, angalia kwenye anwani tovuti ya http://creativecommons.org/licenses/by-sa/4.0 au uandike barua kwa Creative Commons, PO Box 1866, Mountain View, CA 94042, USA.

Biblica® ni alama ya biashara iliyosajilishwa na shirika la Biblica, Inc; unahitaji ruhusa ya kimaandiko kutoka kwa Biblica, Inc. ili kutumia alama ya biashara ya Biblica®. Kulingana na makubaliano ya leseni ya CC BY-SA, unaweza kutoa nakala na kusambaza kazi hii bila kuibadilisha kamwe, mradi tu udumishe alama ya biashara ya Biblica®. Ukibadilisha au kufasiri kazi hii, na hivyo ukanyambua kazi tofauti, sharti uondoe alama ya biashara ya Biblica®. Katika kazi uliyonyambua, sharti uarifu mabadiliko yako, na kutambua kazi yako hivi: "Kazi ya asili ya Biblica, Inc. inapatikana bila bei katika tovuti zawww.biblica.com na open.bible." Ilani ya hakimiliki sharti iwe katika ukurasa wa kichwa au wa hakilimiliki kama ifuatavyo:

Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu™ ONMM™
Hakimiliki © 2018, 2024 na Biblica, Inc.
Biblica® Open Kiswahili Contemporary Scriptures™
Copyright © 2018, 2024 by Biblica, Inc.

"Biblica" ni alama ya biashara iliyosajiliwa katika United States Patent and Trademark Office (ofisi ya hataza na alama za biashara Marekani) na shirika la Biblica, Inc. Imetumiwa na ruhusa.

"Biblica" is a trademark registered in the United States Patent and Trademark Office by Biblica, Inc. Used with permission.

Sharti pia uwasilishe kazi uliyonyambua kupitia kwa liseni hiyo hiyo ya CC BY-SA.

Ikiwa ungependa kujulisha Biblica, Inc. kuhusu tafsiri yako ya kazi hii, tafadhali wasiliana nasi katika tovuti https://open.bible/contact-us.

This work is made available under the Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0 International License (CC BY-SA). To view a copy of this license, visit http://creativecommons.org/licenses/by-sa/4.0 or send a letter to Creative Commons, PO Box 1866, Mountain View, CA 94042, USA.

Biblica® is a trademark registered by Biblica, Inc., and use of the Biblica® trademark requires the written permission of Biblica, Inc. Under the terms of the CC BY-SA license, you may copy and redistribute this unmodified work as long as you keep the Biblica® trademark intact. If you modify a copy or translate this work, thereby creating a derivative work, you must remove the Biblica® trademark. On the derivative work, you must indicate what changes you have made and attribute the work as follows: “The original work by Biblica, Inc. is available for free atwww.biblica.com and open.bible.”

Notice of copyright must appear on the title or copyright page of the work as follows:

Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu™ ONMM™

Hakimiliki © 2018, 2024 na Biblica, Inc.

Biblica® Open Kiswahili Contemporary Scriptures™

Copyright © 2018, 2024 by Biblica, Inc.

“Biblica” ni alama ya biashara iliyosajiliwa katika United States Patent and Trademark Office (ofisi ya hataza na alama za biashara Marekani) na shirika la Biblica, Inc. Imetumiwa na ruhusa.

“Biblica” is a trademark registered in the United States Patent and Trademark Office by Biblica, Inc. Used with permission.

You must also make your derivative work available under the same license (CC BY-SA).

If you would like to notify Biblica, Inc. regarding your translation of this work, please contact us at https://open.bible/contact-us.

This translation is made available to you under the terms of the Creative Commons Attribution Share-Alike license 4.0.

You have permission to share and redistribute this Bible translation in any format and to make reasonable revisions and adaptations of this translation, provided that:

You include the above copyright and source information.

If you make any changes to the text, you must indicate that you did so in a way that makes it clear that the original licensor is not necessarily endorsing your changes.

If you redistribute this text, you must distribute your contributions under the same license as the original.

Pictures included with Scriptures and other documents on this site are licensed just for use with those Scriptures and documents. For other uses, please contact the respective copyright owners.

Note that in addition to the rules above, revising and adapting God's Word involves a great responsibility to be true to God's Word. See Revelation 22:18-19.

2025-05-21

---

PDF generated using Haiola and XeLaTeX on 20 May 2025 from source files dated 21 May 2025

72687ba8-7233-577d-bf23-786df16f869d